UTARATIBU WA KUNUNUA MAZAO YA MIKUNDE

1.0 Utangulizi

Katika msimu wa mauzo 2026/27 Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB), Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Ofisi za wakuu wa Mikoa na Ofisi za Wakuu wa Wilaya husika zitasimamia uendeshaji wa minada ya mazao ya **Choroko,Ufuta, Mbaazi, Dengu, Soya, Njugumawe na Kunde** katika ghala zinazotumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala. Katika msimu huu, mazao hayo yatauzwa kwa njia ya kidigitali kupitia Mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania (OTS) katika Mikoa yote ya Tanzania Bara inayozalisha mazao hayo. Mauzo hayo yanalenga kuleta bei zenye ushindani wa haki, uwazi na kupunguza gharama za ununuzi wa mazao. Wanunuzi wote wanakaribishwa kushiriki kwenye minada itakayoanza hivi karibuni.

2.0 Wajibu wa Mnunuzi

i. Mnunuzi atatakiwa kuzingatia Sheria ya Soko ya Bidhaa 2015, Sheria ya Stakabadhi Ghalani Sura ya 339 (RE) 2016, na Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2013 na Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya mwaka 2023.

ii. Kujaza fomu ya kuridhia kununua mazao kwa utaratibu uliowekwa na TMX na kuiwasilisha TMX kupitia mfumo wa kielektroniki wa mauzo.

iii. Kupitia Katalogi ya Mauzo (Sales Catalogue) na kuweka kiwango cha bei anayotaka kununulia mazao kwa njia ya kielektroniki wakati wa mnada. Kwa maelezo zaidi kuhusu namna ya kutumia mfumo wa kielektroniki wasiliana na TMX kupitia *+255 22 2923700* *+255713298314* au *info@tmx.co.tz* .

iv. Kuweka fedha za Kitanzania ikiwa ni ‘’Kinga ya Dhamana’ kwenye *“settlement accont”* ya Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kinga hii ya dhamana inaweza kutumika kwa zao zaidi ya moja na pia inaweza kutumika kama sehemu ya malipo endapo mnunuzi atashinda kwenye mnada na itarejeshwa kwa mnunuzi pale atapohitaji na kutoa taarifa Soko la Bidhaa.

Jedwali Na. 1: **Viwango vya Kinga ya Dhamana**

Na.	UZITO (TANI)	KIASI (TZS)
1.	1 hadi 30 (kwa wanunuzi wa ndani ya nchi)	5,000,000
2.	30 hadi 50	30,000,000/-
3.	51 Na kuendelea	100,000,000/-

Malipo hayo yafanyike kwenye akaunti ya malipo na uhawilishaji ya TMX:

Jina la Akaunti: **Tanzania Mercantile Exchange**
Benki: **CRDB**
Nambari ya Akaunti: **0150259178501**
Swift Code: **CORUTZTZ**

NB: Mnunuzi atahitajika kulipa gharama ya uendeshaji tofauti na bei ya ununuzi kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

Jedwali Na. 2: Mjengeko wa Tozo kwa mazao Mikunde (Choroko, Mbaazi, Dengu, Soya, Njugumawe na Kunde)

Na	Aina ya Tozo	Kiasi
1	Gharama ya usimamizi Uendeshaji wa vyama vya ushirika	60
2	Mtunza Ghala	37.5
3	Ukaguzi	1.5
4	Dhamana ya utunzaji Mazao Ghalani	4
5	Usafirishaji	40
6	Gharama za Usimamizi Mauzo	5
7	Usimamizi Mkoa	2
8	Usimamizi Wilaya	2
9	Vifungashio	20
10	Maendeleo ya zao	30
Jumla ya tozo		**202 + 3%CESS**

Jedwali Na. 3: Mjengeko wa Tozo kwa Zao la Ufuta

Na	Aina ya Tozo	Kiasi
1	Gharama ya usimamizi Uendeshaji wa vyama vya ushirika	100
2	Mtunza Ghala	37.5
3	Ukaguzi	1.5
4	Dhamana ya Utunzaji Mazao Ghalani	4
5	Usafirishaji	40
6	Gharama za usimamizi wa mauzo	5
7	Usimamizi Mkoa	2
8	Usimamizi Wilaya	2
9	Vifungashio	20
	Maendeleo ya zao	30
Jumla ya tozo		**242 + 3%CESS**

Jedwali Na. 4: Mjengeko wa Tozo kwa mazao ya Mikunde (Choroko, Mbaazi, Dengu, Soya na Ufuta) kwa mikoa itakayofuta utaratibu wa mkusanyaji mazao (*Aggregator)/* Mkulima mkubwa

Na	Aina ya Tozo	Kiasi
1	Mtunza Ghala	38
2	Dhamana ya Utunzaji Mazao Ghalani	5
3	Usafirishaji (Mwekamali)	40
4	Gharama za usimamizi wa mauzo	10
5	Usimamizi Mkoa	2
6	Usimamizi Wilaya	2
7	Vifungashio (mweka mali)	20
8	Maendeleo ya zao	30
Jumla ya tozo		**147 + 3%CESS**

Mnunuzi aliyeshinda katika mnada atatakiwa kutekeleza yafuatayo:

a) Kulipa malipo ya bidhaa aliyonunua ndani ya **siku tatu** (**Saa 72**) za kazi kuanzia wakati anapopokea ankara ya mauzo;

b) Malipo ya bidhaa na tozo zitafanyika kama ilivyoainishwa kwenye Ankara ya mauzo

c) Iwapo Mnunuzi hakufanya malipo ndani ya **saa 72**, mnunuzi atatakiwa kulipa kiasi ambacho hakijalipwa pamoja na adhabu ya asilimia **(5%)** ya kiasi hicho kisicholipwa ndani ya muda usiozidi **saa 24** baada ya kumalizika kwa **saa 72** zilizotajwa kwenye ankara ya mauzo iliyotolewa kwa mnunuzi;

d) Kushindwa kufanya hivyo, mnunuzi atatangazwa kuwa amekiuka masharti na bidhaa hiyo itauzwa tena kwenye mnada mwingine. Kinga ya Dhamana iliyowekwa kwenye akaunti maalamu ya TMX itatumika kufidia wauzaji waliodhurika;

e) Kwa mnunuzi ambaye hakushinda baada ya ombi la maandishi, kinga ya dhamana itarejeshwa kwa mnunuzi ndani ya **masaa 120** siku za kazi.

v. Mnunuzi anatakiwa kuzingatia masharti na vigezo vyote vya kushiriki minada kwa njia ya mtandao kama ilivyoainishwa katika utaratibu huu wa mauzo.

3.0 Hatua ya Uuzaji Mazao

i. Mnunuzi aliyekamilisha hatua ya usajili COPRA na kuweka kinga ya dhamana kwenye akaunti ya Soko la Bidhaa Tanzania anaingizwa kwenye Mfumo wa Mauzo wa Kielektroniki wa TMX;

ii. TMX kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika na Mkaguzi wa Ghala kuhakiki taarifa na kuandaa katalogi ya mauzo (sales catalogue) siku moja kabla ya siku ya mnada, kisha kutumwa kwa wadau mbalimbali;

iii. Taarifa ya katalogi ya mauzo (sales catalogue) itaingizwa kwenye Mfumo wa mauzo wa TMX na mafungu (Lots) kupangwa kwa kuzingatia wingi wa mazao kufuatia upangaji kwenye ghala kuu;

iv. TMX kwa kushirikiana na COPRA, Chama Kikuu cha Ushirika/ mkusanyaji mazao (Aggregator) kukubalina juu ya bei ya kuanzia “Reserve Price” katika mnada husika kulingana na mwenendo wa soko la zao husika na kukiri kuwa bei itakayopatikana juu ya bei anzia itahesabika kuwa amekubali kuuza mazao yake kwa bei hiyo saa moja kabla ya mnada kuanza;

v. Mfumo wa mauzo wa kielekroniki utafunguliwa kwa ajili ya wanunuzi saa moja kabla ya mnada kuanza wenye kupenda kufanya Pre-Bid (Kuweka bei zao kabla ya mnada kuanza) bei hii itaonekana kwa mnunuzi tu mpaka pale muda wa mnada kuanza na mfumo utakapofunguliwa;

vi. Minada itafanyika kwa njia ya kieletroniki (OTS) kwa wanunuzi kushiriki popote walipo kwenye eneo lenye mtandao na endapo kuna wanunuzi walifanya Pre- Bid, bei ya juu iliyopatikana ndio bei itakayoanzia kwenye fungu (lot) husika kwa wanunuzi kuanza kushindana;

vii. Wanunuzi watashindana kununua kwa fungu (Lot) (*Loti* moja ikiwa ni kiasi chote cha mazao uliowasilishwa na Fungu husika au mgawanyo kufuatia wingi wa bidhaa kwenye ghala). *Loti* moja ikitumia muda wa sekunde 60 (dakika 1) na endapo mnunuzi ameweka bei basi itarudi sekunde 45 mpaka ziishe bila mnunuzi mwingine kuweka bei ndipo tutapata mshindi;

viii. **Chama Kikuu cha Ushirika** kuingia kwenye mfumo wa TMX ndani ya **saa moja** na kujaza taarifa ya kuridhia au kukataa bei zilizopatikana baada ya mnada kufanyika;

ix. TMX kwa niaba ya **mkusanyaji mazao** (Aggregator) kuingia kwenye mfumo wa TMX ndani ya **nusu saa** na kujaza taarifa ya kuridhia au kukataa bei zilizopatikana ;

x. Taarifa kwa wadau wengine itatolewa na TMX kwa njia ya kielektroniki ikionyesha kiasi na bei ya mazao yaliyonunuliwa,

xi. Wanunuzi kufanya malipo ya fedha zao ndani ya masaa 72 (siku tatu) toka mauzo kufanyika katika akaunti za malipo kama zilivyo ainishwa kwenye ankara ya mauzo “sales invoice”.

4.0 Usuluhishi wa Migogoro

Mgogoro wa aina yoyote baina ya upande mmoja na mwingine utatatuliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 6 – (1) (b) cha Sheria ya Usalama wa Chakula Sura ya 249 (RE) 2023, Kanuni ya 83 ya Kanuni ya vyama vya ushirika ya mwaka 2015, Sheria ya Stakabadhi Ghalani Sura ya 339 (RE) 2016 na Sheria ya Soko ya Bidhaa 2015.

.....

IMETOLEWA NA AFISA MTENDAJI MKUU SOKO LA BIDHAA TANZANIA

TAREHE 12/02/2026

Tanzania Mercantile Exchange PLC, P.O. Box 31632, Dar es Salaam, TANZANIA,
Email: info@tmx.co.tz, website: www.tmx.co.tz